# TANPAWA

Toleo namba 32 | Jarida la Mtandaoni | Julai 06, 2025




## Mfumo wa Uwekezaji TANESCO - TIMS

- **Mhe. Kapinga Asema** utasaidia kuvutia wawekezaji katika Miradi ya umeme



**RC Chalamila** Apongeza Mkakati wa Vikao Kazi Kati ya **TANESCO** na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa

Ukurasa **6**.



Tanzania Yanadi Sekta ya Miundombinu Maonesho ya **EXPO 2025** Osaka Japan

Ukurasa **14**.

# BODI YA WAHARIRI


| | | |
|---|---|---|
| 01. | Lazaro J. Twange | - Mwenyekiti |
| 02. | Irene Gowelle | - Mhariri Mkuu |
| 03. | Augustino Kasale | - Mhariri |
| 04. | Josephine Maxime | - Mwandishi |
| 05. | Dorina Makaya | - Mwandishi |
| 06. | Charles Kombe | - Mwandishi |
| 07. | Agnes Njaala | - Mwandishi |
| 08. | Gloria Mramba | - Mwandishi |
| 09. | Nurdin Amir Killo | - Mpiga Picha |
| 10. | Costantine James | - Mpiga Picha |
| 11. | Thomas Tito | - Mpiga Picha |
| 12. | Michael Sokotta | - Msanifu Kurasa |




# YALIYOMO
## NDANI YA **JARIDA**


**Ukurasa 4.** Mhe. Kapinga azindua Mfumo wa Uwekezaji wa TANESCO-TIMS

**Ukurasa 6.** RC Chalamila azindua mkakati wa vikao kazi kati ya TANESCO na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa

**Ukurasa 3.** Umeme wa uhakika umechangia ongezeko la Wawekezaji Sekta ya Madini RC Telack

**Ukurasa 8.** TANESCO yaibuka Mshindi wa kwanza mtoa huduma bora Maonesho ya Madini

**Ukurasa 10.** Watanzania Muwe na Imani na TANESCO : MD Twange

**Ukurasa 12.** Mradi wa JNHPP ni Jicho la Watanzania - Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO

**Ukurasa 14.** Tanzania Yanadi Sekta ya Miundombinu Kwenye Maonesho ya Expo 2025 Osaka Japan

**Ukurasa 17.** TANESCO yaanza kampeni ya uhamasishaji ulipaji wa madeni na ulinzi wa miundombinu ya umeme.

**Ukurasa 22.** TANESCO yaibuka Mshindi wa kwanza mtoa huduma bora Maonesho ya Madini

**Ukurasa 23.** Elimu ya Nishati Safi Yawavutia Wananchi Maonesho ya Viwanda, Biashara na Kilimo - Iringa

**Ukurasa 26.** Elimu ya Nishati Safi Iwafikie Wanaume Pia Mwenyekiti Halmashauri ya Kilolo

**Ukurasa 28.** Wananchi Waipongeza TANESCO kwa Elimu ya Nishati Safi ya Umeme ya Kupikia

**Ukurasa 30.** Mradi wa Gridi Imara Msongo wa 220KV Songea Tunduru Wananchi Waanza Kulipwa Fidia Zao

**Ukurasa 33.** Elimu kwa Wateja Yaendelea Kuwakosha Wananchi Kwenye Miradi ya REA Longido - Arusha

**Ukurasa 34.** TANESCO Mkoa wa Kigamboni Yashiriki Katika Sherehe za Mbio za Mwenge wa Uhuru 2025 Wilaya ya Kigamboni

**Ukurasa 35.** Kiongozi wa Mwenge Aipongeza TANESCO Temeke kwa Kuunga Mkono Matumizi ya Nishati Safi

**Ukurasa 38.** Wananchi Mkoa wa Iringa Wafurahia Elimu ya Umeme Kupitia Miradi ya REA Jazilizi

**Ukurasa 40.** Uzinduzi wa Maonesho ya 12 ya Biashara na Utalii Mkoani Tanga

**Ukurasa 41.** TANESCO Yatoa Elimu ya Matumizi ya Nishati Safi kwa Mawakili wa Swerikali - Arusha




# MFUMO WA MPYA WA UWEKEZAJI WA TANECO UTALETA MAPINDUZI YA UWEKEZAJI SEKTA YA UMEME - MHE. KAPINGA

- **Asema utasaidia kuvutia wawekezaji katika Miradi ya umeme**
- **Asisitiza utaongeza uwazi na kupunguza urasimu kwa wawekezaji**

Na **Josephine Maxime,** Dar es Salaam

Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga amesema mfumo mpya wa uwekezaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) unaofahamika kama TIMS yaani (TANESCO INVESTMENT MANAGEMENT SYSTEM) utaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya uwekezaji kwenye sekta ya umeme nchini.

Mhe. Kapinga amesema hayo Juni 25, 2025 wakati akizindua mfumo huo alipomuakilisha Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko ambapo amesema mfumo huo umelenga kuongeza ufanisi na kupunguza urasimu kwa kuwa utamuwezesha muwekezaji kupata taarifa za moja kwa moja kuhusu miradi inayofaa kwa ajili ya uwekezaji kwa haraka na kwa usahihi zaidi.

> *''Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kuweka mazingira mazuri na rafiki kwa uwekezaji. Mifumo kama hii inayotumia teknolojia itasaidia kuondoa urasimu na kutoa nafasi kwa wawekezaji kuwasiliana moja kwa moja na Shirika kwa hatua za haraka zaidi,''amefafanua Mhe.Kapinga.*

Akizungumza kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO Mhandisi Isaac Chanji amesema mfumo huo utaongeza imani kwa wawekezaji wenye nia ya kushiriki miradi ya kimkakati ambapo mpaka sasa jumla ya miradi minne tayari imeingizwa kwenye mfumo huo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw. Lazaro Twange amefafanua kuwa mfumo huo utasaidia kuongeza uwazi, uwajibikaji na kuongeza hofu kwa wale wenye nia ya kufanya uovu kwa sababu kila kitu kinafanyika kwa uwazi.

> *"Zipo nyakati ambazo ofisi za Umma hazisemwi vizuri kutokana na urasimu. Sasa mfumo wa TIMS utaondoa kabisa changamoto hiyo kwakua taarifa zote za fursa za uwekezaji zitajumuishwa na hata wawekezaji wataomba kupitia mfumo huo kwa kuingiza taarifa zao," amesisitiza Bw. Twange.*

Kwa upande wake Naibu Mkurugenzi Mtendaji, Mipango, Utafiti na Uwekezaji, CPA Renatha Ndege amesema kuanzishwa kwa mfumo huo pia kumeakisi mkakati wa TANESCO wa kuendana na matumizi ya teknolojia katika shughuli zake.

Mfumo huu ni miongoni mwa mikakati ya TANESCO ya kuvutia wawekezaji katika sekta ya umeme nchini pamoja na kukuza ushirikiano baina yake na sekta binafsi katika kufanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme nchini.










# RC CHALAMILA AZINDUA MKAKATI WA VIKAO KAZI KATI YA TANESCO NA WENYEVITI WA SERIKALI ZA MITAA

- Awataka Viongozi wa Serikali za Mitaa ya Kinondoni na Ubungo kushirikiana na TANESCO katika ulinzi wa miundombinu ya umeme.
- Ampongeza Mkurugenzi wa TANESCO kwa kuja na mkakati wa kuwashirikisha viongozi hao ambao ni daraja muhimu la mawasiliano kwa wananchi.

**Na Na Gloria Kalist,** Dar es Salaam

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Albert Chalamila amewataka viongozi wa Serikali za Mitaa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kulinda miundombinu ya umeme katika maeneo wanayoyaongoza ili kuzuia hasara kwa Serikali inayotoa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na wananchi.

Mhe. Chalamila ameyasema hayo Juni 24, 2025 wakati akizindua kikao kazi kati ya TANESCO na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa Halmashauri za Manispaa ya Kinondoni na Ubungo ambapo amewataka Wenyeviti hao kushirikiana na Wananchi kulinda mindombinu hiyo na kuwa tayari kusikiliza kero zinazowakabili hasa zinazohusu masuala ya umeme.

> *"Transfoma ikiibiwa umeme ukakosekana mtaa wako. Kiwanda kilichoajiri wananchi kikashindwa kuzalisha, amani itatoweka. Hii ni kwa sababu wafanyakazi hao watashindwa kulipwa kutokana na kutokuwa na uzalishaji. Ndio maana Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO ameona awaite hapa ili mkimuona mtu anaiba Transfoma wajue madhara yake kwa wananchi wanaowaongoza," amesema Mhe. Chalamila.*

Aidha amempongeza Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw. Lazaro Twange kwa kikao kazi hicho huku akiwaasa viongozi hao kuipa ushirikiano menejimenti ya TANESCO katika mitaa wanayoiongoza ili kufanikisha azma ya Serikali ya awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha Watanzania wanapata umeme wa uhakika.

> *"Nawapongeza sana TANESCO kwa kuandaa kikao kazi hiki. Dar es Salaam ni sehemu muhimu ulipo uzalishaji mkubwa wa umeme. Kwa hatua hii ya kuwakutanisha viongozi hawa wa Serikali za Mitaa ni fursa nzuri kwa kuwa wanakutana moja kwa moja na wananchi hivyo ni rahisi kuwabaini hata wale wenye nia ovu ya kuharibu miundombinu ya umeme,"alisisitiza Mhe.Chalamila.*

Nae Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bw. Twange amesema licha ya kufanya kazi kubwa ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme bado Shirika limejizatiti kuhakikisha huduma bora inawafikia wateja kwa haraka na kwa wakati sahihi, akisisitiza mkutano huo pia umelenga kuwa karibu na wananchi kupitia Wenyeviti hao wa Serikali za Mitaa.



*''TANESCO tumejitahidi kuwa karibu na wananchi kupitia kituo chetu cha huduma kwa wateja, tunamshukuru sana Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha Miradi inakamilika na wananchi wanapata umeme wa uhakika. Kazi yetu ni kuendelea kupanga mikakati ya kuhakikisha wananchi wanaunganishiwa umeme na kupata huduma bora,'' liafafanua Bw. Twange.*

Hata hivyo, miongoni mwa matukio mengi, Bw Twange, ametumia sehemu ya Mkutano huo kutoa zawadi ya majiko yanayotumia umeme Kidogo kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Albert Chalamila na baadhi ya Wawakilishi wa Serikali za Mtaa kwa lengo la kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa umeme ikiwa ni ajenda ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.






# UMEME WA UHAKIKA MKOANI LINDI UMECHANGIA ONGEZEKO LA WAWEKEZAJI SEKTA YA MADINI RC TELACK

**Na Na Gloria Mramba -** Ruangwa, Lindi

Muu wa Mkoa wa Lindi, Mhe. Zainab Telack amesema uwepo wa umeme wa kutosha Mkoani Lindi umepelekea kuongezeka kwa idadi ya wawekezaji katika Sekta ya Madini jambo linachagiza maendeleo katika Mkoa huo.

Mhe. Telack ameyasema hayo Juni 11, 2026 katika Halfa ya Uzinduzi wa Maonesho ya Madini yanayofanyika katika Viwanja vya Maonesho ya Madini Wilayani Ruangwa huku akisisitiza dhamira ya Serikali katika kufungua fursa kwa wachimbaji wadogo na kuvutia wawekezaji kwenye Sekta ya Madini nchini.

> *"Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imeshafanikiwa kufikisha umeme katika vijiji vyote vya Mkoa wa Lindi pamoja na baadhi ya vitongoji, huku kazi ya usambazaji ikiendelea. Wakati tunawekeza kwenye madini, hatuwezi kusahau umuhimu wa umeme ambao ni kichocheo kikuu cha maendeleo,"*

Katika hotuba yake wakati wa Ufunguzi wa Maonesho ya Madini , Mhe. Telack alieleza kuwa lengo kuu la maonesho haya ni kuwaunganisha wachimbaji wadogo na wadau mbalimbali wakiwemo wachimbaji wakubwa na wawekezaji, ili kukuza uchumi wa jamii na Taifa kwa ujumla.

> *"Kupitia maonesho haya, tunaamini kuwa tutafungua njia ya ushirikiano, ubadilishanaji wa ujuzi na teknolojia, pamoja na fursa mpya za biashara kwa wachimbaji wetu wadogo," ameongeza Mhe. Telack.*

Aidha, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linashiriki katika maonesho hayo ikiwa ni moja ya mikakati yake ya kufikisha elimu na huduma mbalimbali kwa wananchi pamoja na kuwahakikishia wawekezaji uwepo wa umeme wa uhakika nchini.

Akizungumza katika banda la TANESCO Kaimu Meneja wa TANESCO Mkoa wa Lindi Bw.Theodory Hall amesema kuwa lengo kubwa ni kuunga mkono kauli mbiu iliyobebwa na maonesho hayo isemayo "Madini na Uwekezaji Fursa katika Mkoa wa Lindi". yanapatikakana wakati wote kwa ajili ya uzalishaji.

*"Watu wote wanaowekeza kwenye madini wana uhitaji mkubwa sana wa umeme kwa ajili ya kufanya shughuli zao. Tunawakaribisha wawekezaji mbalimbali ambao wanaziona fursa za madini katika Mkoa wa Lindi kuja na kuweza kuzitumia na sisi tuko tayari kuwahudumia kwakua tuna umeme wa kutosha,"*

*amesema Bw. Hall*

Maonesho haya ya madini yamedumu kwa siku nne kuanzia tarehe 11 hadi 14 Juni 2025 ambapo wananchi, wawekezaji na wadau mbalimbali watapata fursa ya kuona namna Serikali imejipanga kuweka mazingira wezeshi katika kukuza sekta ya madini nchini.





# WATANZANIA MUWE NA IMANI NA TANESCO : MD TWANGE

Na **Charles Kombe,** Dar es Salaam

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Larazo Twange amewataka Watanzania kuwa na Imani na Shirika hilo kwa kuwa wafanyakazi na watendaji wamewekeza nguvu kubwa katika kuwatumikia wananchi katika huduma ya umeme.

Mkurugenzi Twange ameyasema hayo wakati wa ziara yake Mei 16, 2025 katika vituo vya kuzalisha umeme kwa gesi vya Ubungo I, II na III pamoja na Kinyerezi I na Kinyerezi II vilivyopo jijini Dar es Salaam.

> *“Watanzania waendelee kuwa na Imani na Shirika lao la TANESCO na tutaendelea kufanya kazi kwa bidii. Tunafahamu matamanio yao na wakati wote tutajitahidi matamanio hayo yasipotee”, amesema Mkurugenzi Twange.*

Aidha ameishukuru Serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme hapa nchini.

> *“Nimeshuhudia uwekezaji mkubwa wa Serikali. Tunaishukuru sana Serikali kwa kutoa fedha nyingi na tunayo mitambo ya gharama kubwa ambayo inatusaidia kuzalisha umeme”, amesema Mkurugenzi Twange.*

Amewasisitizia watanzania kuwa, wafanyakazi wa TANESCO wanafanya kazi bila kuchoka na yeye kama Mkurugenzi wa Shirika hilo atahakikisha anawawezesha wafanyakazi hao ili kufanya kazi ya kuwapatia umeme wananchi.

> *“Kuna juhudi kubwa zinafanyika usiku na mchana watu hawalali huku, wanakuja kwa awamu ili kuhakikisha Watanzania wanapata umeme. Yale ambayo ni ya kiutawala sisi tutaendelea kuwawezesha kwa wakati ili waweze kufanya kazi zao vizuri na yale ambayo ni makubwa zaidi yanayohitaji kufika nje ya Shirika tutashirikisha Wizara”, ameongeza Mkurugenzi Twange.*

Hii ni miongoni mwa ziara zake za awali tangu kuanza kazi rasmi Mei 9, 2025 baada ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

# MATUKIO KATIKA PICHA

## ZIARA YA MKURUGENZI MTENDAJI WA TANESCO KATIKA VITUO VYA KUZALISHA UMEME KWA GESI - DAR ES SALAAM












# MRADI WA JNHPP NI JICHO LA WATANZANIA MKURUGENZI MTENDAJI WA TANESCO

**Asema kazi iliyobaki ni kuulinda na kuutunza kwa faida ya Watanzania**

Na **Josephine Maxime -** Rufiji

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Lazaro Twange amesema Mradi wa kufua umeme wa JNHPP ambao mpaka sasa umekamilika umekua na mchango mkubwa katika upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini lakini pia unachochea shughuli za kiuchumi.

Twange ameyasema hayo Mei 28, 2025 alipofanya ziara katika mradi huo wa Julius Nyerere ambapo ametoa rai kwa Uongozi wa TANESCO kuhakikisha wanafuatilia vyanzo vya maji vinavyopeleka maji katika Bwawa hilo ili kuhakikisha maji

*"Kama ambavyo tunafahamu Mradi huu umekamilika, Serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha cha zaidi ya shilingi Trilioni 6.5 ,Tunamshukuru sana Mhe Rais Samia kwa kuwezesha Mradi huu kukamilika kazi iliyobaki ni kwetu kuhakikisha Mradi huu unanufaisha kizazi cha sasa na kijacho" amesema Twange*

Pamoja na hayo Mkurugenzi huyo Mtendaji wa TANESCO ameutaka Uongozi wa TANESCO kujenga ushirikiano wa kimkakati na mamlaka za Mkoa na vijiji vilivyopo maeneo husika ili kuhakikisha vyanzo vya maji vinavyopeleka katika Bwawa hilo vinatunzwa na kulindwa kwa maslahi mapama ya Wananchi na Taifa kwa ujumla.

*''Napenda kuwapongeza sana TANESCO, Watanzania wanapaswa kutambua kuwa kuna kazi kubwa sana imefanywa na Wafanyakazi wa TANESCO katika kuchangia mradi huu kukamilika na kuhakikisha wananchi wanapata umeme wa uhakika'' amesisitiza Twange.*

Twange amekuwa na utaratibu wa kutembelea Miradi mbalimbali inayotekelezwa na TANESCO ikiwemo ile ya kupokea na kupoza umeme kwa lengo la kuhakisha Miradi ambayo imekamilika inafanya kazi kwa ufanisi.



# MATUKIO KATIKA PICHA

ZIARA YA MKURUGENZI MTENDAJI WA TANESCO BW. LAZARO TWANGE KATIKA MRADI WA JNHPP - RUFIJI









# TANZANIA YANADI SEKTA YA MIUNDOMBINU KWENYE MAONESHO YA EXPO 2025 OSAKA JAPAN

**Osaka Kansai - Japan**

Tanzania imekuwa kivutio na kupongezwa kwa jitihada kubwa ya Serikali na Sekta Binafsi kuendeleza maeneo ya miundombinu ya ujenzi, mawasiliano na uchukuzi pamoja na miundombinu ya umeme katika maonesho Makubwa ya Dunia ya EXPO OSAKA 2025 katika jiji la Osaka Kansai nchini Japan.

Hayo yameelezwa na Balozi wa Tanzania nchini Japan Mhe. Baraka Luvanda baada ya kufungua rasmi wiki ya miundombinu kwa kukaribisha ushiriki wa Taasisi mbalimbali kutoa maelezo kwa wageni wanaotembelea maonesho hayo ikiwa ni mfululizo wa Programu za kila wiki ambazo zimeandaliwa na TanTrade ili kutangaza fursa katika sekta mbalimbali za kiuchumi zinazosimamiwa na Wizara za Kisekta kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini ya Wizara pamoja na Sekta binafsi kwa uratibu wa TANTRADE kwa kushirikisha Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda-Zanzibar.



Ujumbe wa Tanzania katika wiki ya miundombinu umehusisha ushiriki wa Taasisi mbalimbali ikiwemo TANESCO, Wakala wa Majengo - TBA, TANROADS, TGDC na wengineo.

Mhe. Balozi amesema

> *"...Nimefungua wiki hii ya pili ili kutangaza na kuonesha mambo makubwa ambayo Tanzania imefanya katika sekta ya miundombinu ya barabara, ujenzi, mawasiliano na uchukuzi pamoja na miundombinu ya umeme ili kuitangaza nchi kwa kuvuta wawekezaji zaidi lakini pia kujipanga katika kuzitambua fursa za masoko na Biashara na hivyo kuimarisha uchumi wa nchi. Ni matarajio yetu tutafanikiwa kupata wadau wa miradi mbalimbali ya kimkakati sambamba na fursa za uwekezaji kwenye miradi mbalimbali yenye tija kwa taifa letu..*


Maonesho hayo ya Dunia yameshirikisha nchi zaidi ya 160 ambapo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Kasim Majaliwa ndiye aliyekuwa mgeni rasmi katika maonesho ya Expo 2025 Osaka

# MATUKIO KATIKA PICHA

## TANZANIA YANADI SEKTA YA MIUNDOMBINU MAONESHO YA EXPO 2025 OSAKA JAPAN






TANESCO
LIPA DENI, LINDA MIUNDOMBINU, TUKUHUDUMIE
Huduma Endelevu Huanza na Wewe
Kwa mawasiliano , piga
180 bila malipo




# TANESCO YATANGAZA KUANZA KWA KAMPENI YA UHAMASISHAJI ULIPAJI MADENI NA ULINZI WA MIUNDOMBINU YA UMEME

Na. **Agnes Njaala,** Dar es Salaam

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) limetangaza kuanza kwa kampeni maalumu ya uhamasishaji ulipaji wa madeni na ulinzi wa miundombinu inayokwenda kwa jina la "Lipa Deni, Linda Miundombinu, Tukuhudumie" yenye lengo la kuhamasisha uwajibikaji wa pamoja katika kulipa bili na kulinda miundombinu kwa huduma endelevu ya umeme.

Kampeni hiyo imezinduliwa rasmi , tarehe 19 Juni 2025 na inajikita katika maeneo yote nchini, ambapo kaulimbiu ya kampeni hiyo ni "Huduma endelevu huanza na wewe" ikilenga kuhimiza uwajibikaji wa pamoja kati ya Shirika na wateja wake.

Akizungumza wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliofanyika jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano na Huduma kwa Wateja TANESCO Bi. Irene Gowelle amesema, lengo la kampeni ni kuhimiza wateja wanaodaiwa kulipa madeni yao kwa hiari kabla ya hatua za kisheria kuchukuliwa.

*"Tumefungua milango ya msamaha wa riba, tunawahimiza wateja wetu wenye madeni ya muda mrefu kutumia fursa hii kuweka makubaliano ya ulipaji kwani kufanya hivyo kutawaepusha na hatua za kisheria pamoja na usumbufu wa kusitishiwa huduma," amesisitiza Bi. Irene.*

Sambamba na hilo, ameeleza kuwa TANESCO itafanya pia ukaguzi wa mita za LUKU kwa wateja wa mfumo wa malipo ya kabla, ili kubaini mita zilizochezewa au zenye hitilafu, nakuchukua hatua stahiki kwani wizi wa umeme na matumizi ya mita zilizochezewa ni chanzo cha hasara kwa Shirika unaoathiri ufanisi wa ukusanyaji wa mapato.

Katika hatua nyingine, Bi. Irene amesema kampeni hiyo inajumuisha pia uhamasishaji wa ulinzi wa miundombinu ya umeme kupitia elimu kwa jamii juu ya wajibu wao katika kulinda rasilimali za umma.



*“Ni vema mfahamu kuwa, ulinzi wa miundombinu ya umeme ni jukumu letu sote ni wajibu wa kila mwananchi. Kulinda miundombinu ni kulinda upatikanaji wa huduma endelevu ya umeme kwa wote ili kuchochea uchumi wa nchi na kuwezesha shughuli za kila siku za wateja,” ameeleza Bi. Irene.*

Akifafanua ameeleza kuwa matukio ya wizi wa miundombinu ya umeme yamelisababishia Shirika hasara ya kiasi cha shilingi milioni 770 katika kipindi cha Juni hadi Disemba, 2024 akitaja wizi wa vifaa vya transfoma kukithiri zaidi ambapo idadi ya kesi 63 zimeripotiwa huku mashauri nane (8) yakiwa mahakamani.

Aidha amewahimiza wananchi kushirikiana na vyombo vya usalama kwa kutoa taarifa za uharibifu au wizi wa miundombinu ya umeme ili kuzuia athari na hasara kwa Shirika na jamii kwa ujumla.



Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano na Huduma kwa Wateja

**Bi. Irene Gowelle**

*akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kampeni ya*
***Lipa Madeni, Linda Miundombinu, Tukuhudumie***

## NAMNA KAMPENI YA UHAMASISHAJI ULIPAJI WA MADENI NA ULINZI WA MIUNDOMBINU ILIVYOYAFIKIA MAKUNDI YA WANANCHI MBALIMBALI

### MBEYA



Katika kampeni ya kuendelea kutoa elimu kwenye maeneo mbalimbali mkoani Mbeya, Afisa Uhusiano na Huduma kwa wateja Ndugu Christina Shoki na Afisa Usalama wa Mkoa, Ndugu Aloyce Mndolwa, wakiendelea kutoa elimu kwenye vijiji, vitongoji na maeneo yenye mikusanyiko mkubwa juu ya umuhimu wa ulipaji wa madeni kwa hiari na ulinzi wa miundombinu.

### MANYARA



Afisa Usalama Mkoa Manyara Davis Mkwiche na Afisa Uhusiano Mkoa Samuel Mandari wamefanya Mikutano kwenye Kata ya Magugu wilayani Babati katika Vijiji vya Masware, Sarame na Magugu ambapo wananchi waliohudhuria katika mkutano huo walielimishwa juu ya Utekelezaji wa Miradi ya umeme ,Taratibu za kujiunga na Huduma ya umeme, Ulipaji wa Madeni pamoja na Ulinzi na Usalama wa Miundombinu.

## PWANI



TANESCO Mkoa wa Pwani June 17 imetoa elimu ya ulinzi na utunzaji miundombinu kwa wakazi wilaya ya Mkuranga katika kijiji cha Kimazichana kitongoji cha Nyamla ambapo Wafanyakazi wa TANESCO kutoka Pwani Kaskazini na Pwani Kusini walishirikiana kutoa elimu ya umuhimu wa ulinzi na utunzaji wa miundombinu ya Shirika hasa mashine umba na nyaya za kusambaza umeme.

## MBURAHATI



Elimu ya ulipaji wa madeni na ulinzi wa miundombinu ya umeme ilivyowafikia waendesha bodaboda Mburahati.

## SONGWE



Shirika la umeme Tanzania TANESCO Mkoa wa Songwe limeanza rasmi zoezi la utoaji elimu kwa wananchi/kwenye mikusanyiko ya watu kwa ushirikiano wa Afisa Usalama Bw. Juma Mahuba, pamoja na Afisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja Bi. Elfrida Nsulau ambapo elimu hiyo imetolewa kwa wananchi wa Mkoa wa Songwe wilaya ya Ileje pamoja na Mbozi juu ya Ulinzi wa Miundombinu ya Umeme, pamoja na Usalama wa Umeme.

## RUKWA



Wananchi Rukwa wakiendelea kupatiwa elimu ya ulipaji wa madeni na ulinzi wa miundombinu ya umeme



# TANESCO YAIBUKA MSHINDI WA KWANZA MTOA HUDUMA BORA MAONESHO YA MADINI

Na **Gloria Kalist,** Ruangwa, Lindi

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) limeibuka mshindi wa kwanza wa Tuzo ya Utoaji wa Huduma Bora kwa Wateja katika Mkoa wa Lindi kwenye Maonesho ya Madini (Mining Expo 2025) yaliyofanyika katika Viwanja vya Maonesho Wilayani Ruangwa.

Tuzo hiyo imekabidhiwa kwa TANESCO na Naibu Waziri wa Madini Mhe. Dkt. Steven Kiruswa katika hafla ya kilele cha maonesho hayo na kupokelewa na Kaimu Meneja wa TANESCO Bw. Theodory Hall.

Maonesho hayo yaliyoandaliwa na Wizara ya Madini, yalianza rasmi Juni 11, 2025 na kuhitimishwa Tarehe 14 Juni, 2025 yalilenga kuwakutanisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Madini ikiwemo wachimbaji wadogo na wakubwa, wawekezaji, Taasisi za Serikali, Taasisi Binafsi, watoa huduma pamoja na wananchi.

TANESCO kama mmoja wa washiriki wa maonesho hayo, ilitumia jukwaa hilo kuonesha utekelezaji wa miradi yake ya kimkakati ya Uzalishaji na Usambazaji wa Umeme pamoja na kutoa elimu kuhusu huduma zake kwa wananchi na wadau mbalimbali ikiwemo Nishati Safi ya Umeme ya Kupikia.

Maonesho hayo ni sehemu ya Mkakati wa Serikali kuimarisha Sekta ya Madini na kuchochea maendeleo ya kiuchumi kupitia ushirikiano kati ya wadau mbalimbali wa Sekta hiyo, zikiwemo Taasisi zinazotoa huduma muhimu kama TANESCO.

Aidha kupitia ushiriki wake, TANESCO imedhihirisha dhamira yake ya dhati katika kusogeza huduma karibu na wananchi, na kuendelea kuwa mshirika muhimu katika safari ya maendeleo ya Uchumi wa Taifa.






# ELIMU YA NISHATI SAFI YAWAVUTIA WANANCHI MAONESHO YA VIWANDA, BIASHARA NA KILIMO IRINGA

- **Wasema wako tayari kuachana na matumizi ya kuni na mkaa**
- **Waipongeza TANESCO kwa kuanzisha namba mpya 180 bila malipo**

Na **Josephine Maxime,** Iringa

Baadhi ya wananchi waliotembelea banda la TANESCO katika maonesho ya Viwanda, Biashara na Kilimo yaliyofanyika katika Wilaya ya Kilolo Mkoani Iringa wamekiri kuwa elimu waliyoipata juu ya matumizi ya nishati ya umeme kwa ajili ya kupikia ni mapinduzi makubwa ya kuachana na matumizi ya kuni na mkaa ambayo yana athari kiafya na kimazingira.

Akizungumza mara baada ya kutembelea banda hilo katika Halmashauri ya mji mdogo wa Ilula kwenye viwanja vya Chuo cha Maendeleo ya wananchi FDC Mei 21, 2025 mkazi wa Ilula Bw. Autosi Fabiani amesema kilichomsukuma kufika katika banda la TANESCO ni baada ya kusikia uwepo wa majiko yanayotumia umeme kidogo hatua ambayo imempa nguvu ya kuachana na matumizi ya kuni na mkaa kama nishati ya kupikia.

> *Nimefurahi sana kupata elimu hii kumbe hata sisi wakulima tunaweza kutumia umeme kupikia, nina amini elimu hii ikiendelea kuwafikia wananchi wengi hakuna mwananchi atakayetaka Kwenda porini kuhangaika na kuni,'' amefafanua Bw. Autosi*

Naye Afisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja Iringa Donasian John amesema TANESCO ni mdau mkubwa katika maonesho hayo kwa kuwa nishati ya umeme inahusika moja kwa moja katika masuala ya uzalishaji kupitia viwanda, bishara na kilimo lakini pia ni nguzo muhimu katika kuvutia uwekezaji nchini.

> *''TANESCO tuko mahali hapa kama mdau mkubwa kwa kuwa tunaingia kwenye Sekta zote zinazohusika katika maonesho haya, kwenye viwanda bila nishati ya umeme hakuna uzalishaji,kwenye kilimo tunaingia kwa kuwa umwagiliaji unahitaji umeme,na kwenye biashara bila umeme hakuna uwekezaji '' amesisitiza Bw. Donasian*

Maonesho haya ya Viwanda,Biashara na Kilimo yamefanyika katika Halmashauri ya mji mdogo wa Ilula Wilayani Kilolo Mkoani Iringa ambayo yalianza rasmi Mei 21 na kumalizika Mei 25 mwaka huu.

# MATUKIO KATIKA PICHA

## NAMNA ELIMU YA NISHATI SAFI ILIVYOWAVUTIA WANANCHI KATIKA MAONESHO YA VIWANDA, BIASHARA NA KILIMO IRINGA







# Umeme **Nishati** Nafuu Zaidi **Jikoni,** Pika kwa **Umeme**

Ni Gharama Nafuu

Itakufupishia Muda Jikoni

Ni Salama kwa Afya na Mazingira




Pika kwa Umeme



# ELIMU YA NISHATI SAFI IWAFIKIE WANAUME PIA MWENYEKITI HALMASHAURI YA KILOLO

**Asema matumizi ya umeme yanaruhusu mtu yoyote kupika kwa unadhifu**

Na **Josephine Maxime,** Iringa

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo Mkoani Iringa Mhe. Anna Msola ametoa rai kwa Shirika la umeme Tanzania, TANESCO kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa umeme hata kwa wanaume kwa kuwa mazingira yake yanaruhusu mtu yoyote kupika akiwa nadhifu.

Akizungumza Mei 24,2025 mara baada ya kutembelea Banda la TANESCO katika Maonesho ya Viwanda, Biashara na Kilimo Mkoani Iringa, Mhe. Msola licha ya kuipongeza TANESCO kwa jitihada zake za kutekeleza ajenda ya Serikali ,amesema ni wakati sasa elimu hiyo iwafikie wanaume na hii ni baada ya wanawake wengi kuonekana kuelewa na kuanza kuchukua hatua ya kubadili mitazamo.

> *''Elimu ya nishati safi ya kupikia imewafikia wananchi wengi na kwa kweli Faida zake tumeziona. Napenda kutoa rai kwa TANESCO kuendelea na jitihada hizo ,haya ni mapinduzi makubwa na imekua chachu kwa baadhi ya wanaume kuingia jikoni kusaidiana na wake zao kupika''alisema Mhe. Msola.*

Naye mkazi wa Ilula Bw Samweli Kajiba aliyetembelea maonesho hayo ameishukuru TANESCO kwa uharaka wao wa kutoa taarifa mapema pale panapojitokeza changamoto yoyote ya upatikanaji wa umeme.

TANESCO imekuwa ikitumia Maonesho hayo ya Viwanda, Biashara na Kilimo yanaliyofanyika katika Halmashauri ya mji mdogo wa Ilula Mkoani Iringa kama jukwaa maalumu la kutoa elimu kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Shirika hilo kwa wananchi waliotembelea maonesho hayo.



# MATUKIO KATIKA PICHA

MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO MHE. ANNA MSOLA AKIHAMASISHA ELIMU YA NISHATI SAFI KUWAFIKIA NA WANAUME PIA









# WANANCHI WAIPONGEZA TANESCO KWA ELIMU YA NISHATI SAFI YA UMEME YA KUPIKIA

**Wasema ni muhimu kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya nishati ya umeme kupikia.**

Na **Gloria Mramba,** Dar es Salaam

Baadhi ya wananchi Jijini Dar es saalam wamelipongeza Shirika la Umeme Tanzania TANESCO kwa kuwapa elimu mbalimbali ikiwemo ya matumizi ya Nishati safi ya umeme kupikia hali ambayo imekuwa chachu ya kuhamasisha matumizi ya Nishati safi Nchini.

Wamebainisha hayo Mei 29. 2025 katika Maonesho ya wiki ya Nishati Jadidifu 2025 yaliyofanyika katika Ukumbi wa kimataifa wa Julius Nyerere uliopo jijini Dar Es Salaam ambapo TANESCO imetumia nafasi hiyo kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Nishati Jadidifu inayolenga kuongeza uzalishaji wa umeme nchini.

Wamesema kuwa wananchi wengi walikuwa wanaogopa kutumia Nishati ya Umeme Kupikia wakihofia gharama kubwa lakini kwa elimu waliyoipata imewasaidia kwa kiasi kikubwa kuhamasika na matumizi ya Nishati safi ya umeme Kupikia.

Akizungumza katika banda la TANESCO, Mhandisi wa Umeme Idara ya Utafiti TANESCO Mhandisi Caritas Rwiza amesema mwitikio wa wananchi pamoja washiriki wa Mkutano wa Nishati Jadidifu 2025 katika Banda la TANESCO umekuwa Mkubwa hivyo wametumia nafasi hiyo kutoa elimu ya matumizi ya Nishati ya Umeme kupikia pamoja kuelezea miradi mbalimbali ya Umeme Jadidifu.

> *"Sisi kama TANESCO tumeweza kupata nafasi ya kutoa elimu ya miradi yetu mbalimbali ya Nishati Jadidifu ambayo ipo katika hatua ya utekelezaji katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo Shinyanga lakini pia tumehamasisha matumizi ya Nishati safi ya Umeme kupikia kwa wananchi"*

Kwa upande wake Meneja Tafiti na Ubunifu kutoka Kampuni Tanzu ya TANESCO (TGDC) Mhandisi Mkufu Tindi amesema katika kuongeza hali ya uzalishaji wa umeme nchini kupitia miradi ya Umeme jadidifu Tanzania inauwezo wa kuzalisha Megawati elfu 5,000 za umeme kwa ajili ya matumizi ya moja kwa moja ili kurahisisha upatikanaji wa umeme nchini.

Amesema Tanzania ina mikoa zaidi ya 15 yenye vyanzo vya Nishati ya Umeme wa Joto ardhi na Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania chini ya Kampuni tanzu ya TGDC imeanza kutekeleza miradi hiyo kwa kuanza na miradi ya kipaumbele mitano ikiwemo mradi wa Ngozi unaotarajia kuzalisha Megawati 70.

# MATUKIO KATIKA PICHA

TANESCO NA KAMPUNI YAKE TANZU TGDC YASHIRIKI WIKI YA NISHATI JADIDIFU 2025, DAR ES SALAAM








# MRADI WA GRIDI IMARA MSONGO WA 220KV SONGEA TUNDURU WANANCHI WAANZA KULIPWA FIDIA ZAO



Shirika la Umeme Tanzania TANESCO, Mei 28, 2025 limeanza kuwalipa fidia Wananchi wanaoishi Mtaa wa Mlete Kata ya Shule ya Tanga Manispaa ya Songea Mkoani Ruvuma, Fidia inayotokana nakupisha Maeneo yao kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Gridi Imara Msongo wa 220KV Songea -Tunduru, katika Kuhakikisha Umeme wa Uhakika wa Grid ya Taifa unafika kwenye Maeneo tajwa nakuchochea Shughuli za Kiuchumi kwa Wananchi.

Maafisa wa TANESCO Kutoka makao makuu wamefika Mlete ilipo Ofisi ya Mtaa, ambako zoezi la kukabidhi hundi na kuwafungulia akaunti Wananchi likifanyika ambapo Shilingi bilioni 2.5 zimelipwa kwa wananchi wote waliopitiwa na njia hiyo ya umeme.

Mradi huu wa kuunganisha mikoa ya kusini na Gridi ya Taifa utasaidia kuwa na umeme wa uhakika na kuchochea shughuli za maendeleo zinazotegemea umeme kwenye mikoa ya kusini.



# MATUKIO KATIKA PICHA

WANANCHI WAANZA KULIPWA FIDIA BAADA YA KUPISHA MRADI WA GRIDI IMARA WA MSONGO WA 220 KV SONGEA - TUNDURU







# UNAWEZA KUONA TOKEN ZAKO ZA UMEME KUPITIA GePG APP

## Ndugu Mteja!

Endapo utakuwa umenunua umeme na haujapata **token** au umezifuta unaweza kuziona kwa kupitia **GePG** App

### KUONA UMEME WAKO ULIONUNUA FATA TARATIBU ZIFUATAZO




1. Pakua GePG App
2. Ingia kwenye menu ya GePG kwenye simu yako
3. Chagua LUKU
4. Chagua get last token ( ona umeme wa mwisho)
5. Chagua unataka kuona kwa kutumia namba ya simu uliyonunulia umeme au Namba ya Mita au Namba ya risiti
6. Ingiza namba ya mita au namba ya simu au namba ya risiti
7. Bofya Wasilisha ( Submit)
8. Token za umeme wako ulizonunua hivi karibuni zitaonekana
9. Bofya mshale wa token husika kuone maelezo zaidi (Umenuna lini, kiasi, token husika nk)

www.tanesco.co.tz



# ELIMU KWA WATEJA YAENDELEA KUWAKOSHA WANANCHI KWENYE MIRADI YA REA LONGIDO ARUSHA

Timu ya huduma kwa wateja TANESCO Mkoa wa Arusha imeendelea kutoa elimu kwa wanufaika wa Miradi ya REA katika Wilaya ya Longido katika vijiji vya Darajani, Engaranaibour, na Mundarara.

Elimu hiyo imetolewa June 4 2025, ambayo imelenga kuwawezesha wananchi kufahamu taratibu mbalimbali za shirika na kujibu maswali ya papo kwa papo ambapo pia wananchi walielimishwa kuhusu matumizi ya namba mpya bila malipo ya 180 ili kutoa taarifa na maulizo yoyote kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na TANESCO

Kwa mujibu wa Afisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja Arusha James Vesso mbali na elimu hiyo pia wananchi wamejengewa uwezo kuhusu gharama za kuunganishiwa umeme ili kuhakikisha huduma hiyo muhimu inawafikia wananchi wengi kulingana na mahitaji yao.






# TANESCO MKOA WA KIGAMBONI YASHIRIKI KATIKA SHEREHE ZA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2025 WILAYA YA KIGAMBONI

TANESCO Mkoa wa Kigamboni imeshiriki katika sherehe za Mbio za Mwenge wa Uhuru 2025 zilizofanyika June 2 2025, katika Viwanja vya Tungi Mnadani, Wilaya ya Kigamboni.

Sherehe hizo zilihudhuriwa na wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kigamboni, wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo Mhe. Halima Bulembo.

Katika kushiriki mbio hizo TANESCO Kigamboni, imetumia fursa hiyo muhimu kutoa Elimu kwa wananchi kuhusu Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa Umeme ikiwa ni sehemu ya jitihada za kusaidia kulinda mazingira na kuboresha afya za watumiaji wa nishati majumbani.



Aidha, TANESCO ilihamasisha wananchi kuhusu matumizi ya Namba mpya ya huduma kwa wateja 180 ambayo ni ya bila malipo, ili kurahisisha mawasiliano kati ya wananchi na shirika hilo.

Hata hivyo TANESCO Kigamboni inaendelea kujivunia kuwa sehemu ya jamii na kuunga mkono jitihada mbalimbali za maendeleo, hususani zile zinazolenga kuhamasisha Umuhimu wa Nishati safi kwa wananchi na wateja.





# KIONGOZI WA MWENGE AIPONGEZA TANESCO TEMEKE KWA KUUNGA MKONO MATUMIZI YA NISHATI SAFI

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Bw. Ismail Ali Ussi, amelipongeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Temeke kwa kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, za kuhamasisha Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kupitia majiko janja yanayotumia umeme kidogo.

Akizungumza Juni 1, 2025, jijini Dar es Salaam wakati alipotembelea Banda la TANESCO katika hafla ya mapokezi ya Mwenge wa Uhuru iliyofanyika katika Viwanja vya TANESCO Wilaya ya Yombo, Bw. Ussi amesema kuwa ni muhimu kwa jamii kutumia Nishati Safi ya Umeme kwani ni rafiki kwa afya na mazingira.

> *"Majiko janja yanayotumia nishati ya umeme ni rafiki wa mazingira na yanatumia Unit chache za umeme. Nimeridhishwa na utekelezaji wa miradi yote katika Manispaa ya Temeke, ni muhimu kuwajibika katika utekelezaji wa miradi ili kufikia malengo ya maendeleo,"*
>
> *amesema Bw. Ussi.*

Kwa upande wake, Afisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja Mkoa wa Temeke, Bw. Goodluck Assenga, amesema kuwa majiko hayo yanaweza kutumika majumbani na katika maeneo ya biashara kama vile hoteli kwani ni gharama nafuu na salama kwa mazingira na afya ya watumiaji ambapo pia ametoa wito kwa wananchi kuchangamkia fursa ya kununua majiko hayo sanifu.

Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2025 umebeba kaulimbiu isemayo: "Jitokeze Kushiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kwa Amani na Utulivu." Ambapo Wilaya ya Temeke imeupokea Mwenge huo kutoka Mkoa wa Lindi.



# MATUKIO KATIKA PICHA

KIONGOZI WA MWENGE AIPONGEZA TANESCO TEMEKE KWA KUUNGA MKONO MATUMIZI YA NISHATI SAFI






TANESCO
180
Mchongo ni
Piga bure tukuhudumie
Namba yetu mpya ya huduma
kwa **wateja** bila malipo.
www.tanesco.co.tz



# WANANCHI MKOA WA IRINGA WAFURAHIA ELIMU YA UMEME KUPITIA MIRADI YA REA JAZILIZI

Wananchi kijiji cha Ndiwili, Mkombilenga, Nyabula na Tagamenda katika Wilaya ya Iringa vijijini wamefurahia kupata elimu ya umeme kupitia miradi ya REA JAZILIZI ambapo timu ya huduma kwa wateja ya Mkoa wa Iringa imefanikiwa kutoa elimu katika kitongoji cha Matema, Migori A, Mtakuja, Ilutila, Ikalagasi, Igodikafu na Kihondo ili kuwawezesha kufahamu njia sahihi za kuomba hadi kupata huduma za umeme kwa Usalama kupitia miradi ya REA.

Aidha wakazi wa vitongoji hivyo walipata elimu juu ya namba mpya ya huduma kwa wateja ambayo mteja ataweza kupiga simu pindi apatapo changamoto ya Umeme pasipo kutozwa gharama yoyote.

Pamoja na mambo mengine wananchi hao pia wameelimishwa kuhusu viashiria vya usalama na Mambo muhimu ya kuzingatia kujiongezea usalama na kuepuka majanga yatokanayo na umeme kwa kutumia wakandarasi wenye leseni.



# MATUKIO KATIKA PICHA

## WANANCHI IRINGA VIJIJINI WAKIPATIWA ELIMU YA UMEME KUPITIA MIRADI YA REA JAZILIZI









# UZINDUZI WA MAONESHO YA 12 YA BIASHARA NA UTALII MKOANI TANGA

Maonesho ya 12 ya Biashara na Utalii yaliyofanyika Mkoani Tanga, yamelenga kutoa fursa kwa Taasisi, wafanyabiashara na wajasiriamali ili kubadilishana uzoefu, kuonesha bidhaa na huduma zao, pamoja na kujenga mahusiano ya kibiashara yatakayochangia kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mgeni rasmi katika uzinduzi huo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Mheshimiwa Dadi Kolimba, ambaye alitembelea mabanda ya washiriki mbalimbali wakiwemo kutoka Taasisi za Umma, Taasisi binafsi pamoja na wajasiriamali.

Miongoni mwa mabanda aliyotembelea ni banda la Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Tanga, ambapo alipokelewa na Meneja wa TANESCO Mkoa wa Tanga, Mhandisi Hadija Mbaruku.

Mhandisi Mbaruku alitoa elimu juu ya Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, huduma ya namba mpya bila malipo ya 180, pamoja na taarifa kuhusu miradi mbalimbali ya umeme inayotekelezwa na TANESCO kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Mheshimiwa Kolimba aliipongeza TANESCO kwa juhudi kubwa wanazofanya katika kuhakikisha huduma ya umeme inawafikia wananchi kwa ufanisi






# TANESCO YATOA ELIMU YA MATUMIZI YA NISHATI SAFI KWA MAWAKILI WA SERIKALI - ARUSHA

**Wasisitizwa kuwa mabalozi wa kutumia Nishati ya Umeme kupikia.**

Mawakili wa Serikali June 3 2025, wamepatiwa elimu kuhusu Matumizi ya Nishati Safi ya Umeme kwa ajili ya kupikia ikiwa ni muendelezo wa kampeni inayofanywa na TANESCO kwa makundi mbalimbali ili kufikia azma ya Serikali ya kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia Nishati Safi ya Kupikia ifikapo mwaka 2034.

Akitoa elimu hiyo Mkoani Arusha mbele ya Mawakili hao Bi. Adelina Lyakurwa Afisa Masoko kutoka TANESCO amesema Shirika hilo limejikita katika kuhakikisha watanzania wengi wanaelimishwa kuhusu Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia hasa ya Umeme kwa kuwa nishati hiyo imeonekana kuwa ni nafuu zaidi kulinganisha na zingine

*"Sisi TANESCO tunaungana na Ajenda ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, tunatambua zipo nishati nyingi za kupikia lakini umeme ni nishati nafuu zaidi ya kupikia tunawahamasisha kuwa mabalozi kwa wengine ambao bado hawajafikiwa na elimu hii,alisisitiza Bi Adelina*

Nae Mkazi wa Arusha Bw. Juma Yusuph ameipongeza TANESCO kwa kuwa na mkakati wa kutoa elimu hii kwa kuwa vifaa vinavyotumika katika matumizi ya kupikia vinaendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia na ni rafiki wa mazingira

TANESCO imeutumia Mkutano huo wa Mawakili ulioanza June 2 hadi 6 uliofanyika Mkoani Arusha kutoa elimu kuhusu Matumizi ya Nishati Safi ya Umeme kupikia na shughuli mbalimbali zinazofanywa na Shirika hilo.



# MATUKIO KATIKA PICHA

TANESCO YATOA ELIMU YA NISHATI SAFI KWA MAWAKILI WA SERIKALI - ARUSHA









# TANESCO YAPEWA TUZO YA UDHAMINI WA MAFUNZO YA MAWAKILI WA SERIKALI - ARUSHA





# TANESCO NA USHIRIKIANO WA WADAU

## **NMB** Mbezi Beach Wahamia Kwenye Matumizi ya Nishati Safi ya Umeme Kupikia

Mtimu ya Huduma kwa Wateja na Usalama kutoka TANESCO – Mkoa wa Kinondoni Kaskazini Juni 18 imefanya kampeni maalum ya elimu kwa Wafanyakazi wa NMB Tawi la Mbezi Beach kuhusu Usalama wa Miundombinu ya Umeme na masuala mbalimbali yanayohusu TANESCO



Wafanyakazi hao wa NMB pia wameelimishwa juu ya matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa Umeme kama ni nafuu zaidi jikoni kulinganisha na nishati zingine.



Pata **Taarifa** na **Huduma** Mbalimbali Kupitia **Mitandao** Yetu ya **Kijamii**




@tanesco_official_page

@tanescoyetu

@tanescoyetutz

www.tanesco.co.tz

0758 346 869